

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

Telegram: "MAWASILIANO"
Simu: 255 26 2324513
Nukushi: 255 26 23211027
Barua Pepe: ps@mawasiliano.go.tz
Tovuti: www.mcit.go.tz



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Ujenzi,
S.L.P. 677,
40470 DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA KUTOA MAONI KWENYE MAREKEBISHO YA KANUNI ZA LESENI NA KANUNI ZA MIUNDOMBINU YA UTANGAZAJI

Dodoma- Agosti 19, 2021

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile, anawakaribisha wadau wa Sekta ya Mawasiliano nchini kutoa maoni katika rasimu za marekebisho ya Kanuni za Leseni za mwaka 2018 na Kanuni za Miundombinu ya Utangazaji za mwaka 2018 (*The Electronic and Postal Communications (Digital and Other Broadcasting Networks and Services) Regulations 2018 and (the Electronic and Postal Communications (Licensing) Regulations 2018*).

Marekebisho haya yamefanywa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 165 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010. Maboresho hayo yatazifanya Kanuni hizo ziendane na maendeleo ya teknolojia pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano na habari kwa wananchi.

Rasimu za marekebisho ya Kanuni hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara (www.mawasiliano.go.tz) pamoja na tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA (www.tcra.go.tz). Maoni yawasilishwe kwa anuani za barua pepe zifuatazo: prisca.ulomi@mawasiliano.go.tz na ramadhani.jongo@mawasiliano.go.tz

Pia, Wizara inawakaribisha wadau wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nchini kuhudhuria mkutano wa wadau utakaofanyika tarehe Agosti 26, 2021 katika Ukumbi wa PSSF (zamani - LAPF) Jijini Dodoma, kuanzia Saa 2.00 asubuhi ili kuhitimisha zoezi la utoaji maoni. Wote mnakaribishwa.

Imetolewa na: -

A blue ink signature of Prisca J. Ulomi, consisting of a stylized 'P' and 'U' intertwined.

Prisca J. Ulomi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari